



Maswali

1. Baada ya nabii Eliya nani alichukuwa nafasi yake?
2. Eliya na Elisha walivuka mto namna gani?
3. Elisha aliuliza apewe nini?
4. Eliya alijibu nini?
5. Elisha aliona nini angani?
6. Nini ilifanyika kwa Eliya?
7. Eliya aliangusha nini?
8. Elisha alivuka Mto wa Yordani namna gani?
9. Eliya aliandikia nani baadaye?
10. Mungu alipea Elisha nini?

Majibu

1. Elisha alikuwa nabii baada ya Eliya.
2. Eliya alipiga maji na joho lake. Maji yaligawanyika.
3. Elisha aliomba Eliya ampe nguvu za Mungu maradufu.
4. Kama Elisha angeona Eliya akichukuliwa, angepata nguvu za Mungu.
5. Elisha aliona gari na farasi za moto.
6. Eliya alichukuliwa kwa upepo wa kisulisuli.
7. Eliya aliangusha joho lake.
8. Elisha alipiga mto kwa joho la Eliya. Maji yaligawanyika.
9. Eliya aliandikia Yoram, mkwewe Ahabu barua.
10. Mungu alimpa Elisha nguvu zake maradufu.

72 Eliya anaacha Elisha

Kwa Biblia

2 Wafalme 2:1–17

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alituma nabii mwingine kufundisha watu. Mungu alikuwa na Elisha kwa sababu alimwamini

Somo

Eliya aliendelea kuwa mzee. Bunde tu, wakati ungefika wenye hangeweza kufanya kazi kama nabii wa Mungu. Ilikuwa la muhimu kama kungekuwa na nabii mwingine mzuri wa kumfuata na afundishe watu kupenda na kumtii Mungu.

Mungu alimwambia Eliya kwamba amemchagua nabii mwingine. Elisha angekuwa nabii baada yake. Elisha angeendeleza kazi ya Eliya. Elisha angefundisha watu juu ya Mungu.

Elisha alisafiri na Eliya. Alisaidia Eliya na kazi zake. Eliya alifundisha Elisha kuenenda kwa njia za Mungu. Alifundisha Elisha juu ya Mungu na sheria zake.

Siku moja Mungu alimwambia Eliya kwamba ilikuwa siku yake ya mwisho kuwa nabii. Eliya alienda kwa shule ya manabii kuwaaga. Elisha alienda naye. Mungu aliambia manabii vijana kwamba hiyo ilikuwa siku ya Eliya ya mwisho. Eliya aliwaaga heri njema.

Halafu Eliya akaenda na Elisha kwa Mto wa Yordani. Hakukuwa na daraja ya kuvuka huo mto. Eliya alikuwa na nguvu za Mungu. Aliomba Mungu.

Alitoa joho lake. Alilikunja kunja na kupiga maji nalo. Maji yaligawanyika halafu Eliya na Elisha wakavukia kwa nchi kavu. Baadaye maji yalirudi.

Eliya na Elisha waliendelea kutembea pamoja. Eliya aliuliza Elisha, “Nikufanyie nini?” Elisha alijua kwamba itakuwa vigumu kuwa nabii wa Mungu baada ya Eliya kuondoka. Watu wengi walikuwa bado wanaabudu Baali. Lazima afundishe watu kumjua Mungu.

Eliya alikuwa na nguvu za Mungu zilizomwezesha kufanya miujiza. Hii ilimsaidia kufundisha watu maneno ya Mungu. Elisha alijibu, “Nipe nguvu za Mungu. Nipe hizo nguvu maradufu ya zako.” Eliya alimwambia, “Umeuliza kitu kigumu. Ukiniona nikiondolewa kwako, inamaanisha utazipata.”

Eliya na Elisha waliendelea kutembea pamoja. Eliya alimwambia maneno mengi sana kama wasia utakaomsaidia. Bunde tu Elisha aliona gari na farasi za moto angani. Hilo gari la moto lilikuja katikati ya Eliya na Elisha. Kulitokea upepo wa kisulisuli uliochukuwa Eliya juu angani. Elisha alitoa sauti, “Magari na wapanda farasi wa Israeli.”



Elisha alikasirika kwa sababu Eliya ameenda. Alikuwa na wasi wasi juu ya kazi ngumu ya kufanya kama nabii wa Mungu. Ingekuwa vigumu kuifanya bila Eliya kumsaidia. Elisha aliangalia chini. Aliona kwamba Eliya alikuwa ameangusha joho lake. Alikumbuka ahadi ya Eliya. Elisha alikuwa ameona Eliya akichukuliwa.

Alikuwa ameona nguvu za Mungu ndani ya gari na farasi ya moto. Mungu angempa uwezo wa kufanya miujiza. Angeweza kuonyesha watu kwamba Mungu ni Mungu wa kweli. Mungu angekuwa naye na amsaidie. Elisha alikuwa tayari kuanza kazi yake.

Elisha alianza safari ya kurudi kwa Mto wa Yordani. Alipiga maji kwa joho la Eliya. Mto uligawanyika na akavuka kwa nchi kavu. Manabii vijana walikuwa wamemngojea. Waliona vile alivuka mto. Walijua kwamba ana nguvu za Mungu. Walijua kwamba sasa Elisha ni nabii wa Mungu. Yeye ndiye kiongozi wao mpya.

Kazi ya Eliya kama nabii ilifika mwisho. Mungu alimpeleka pahali pengine atulie kule mpaka afe. Manabii vijana walituma watu hamsini kumtafuta Eliya kila pahali lakini hawakumpata. Mungu alimchukua. Baada ya muda aliandikia mfalme Yoram, mkwewe Ahabu barua. Yoram alikuwa mfalme muovu. Eliya alimwandikia ujumbe kutoka kwa Mungu. (2 Mambo ya Nyakati 21:12 – 15)

Yoram,
Mungu amekukasirikia
wewe kwa sababu
umongoza watu
kuabudu miungu na
umewaua ndugu zako.
Mungu ataleta wewe
na familia yako
ugonjwa wa tauni.
Nabii Eliya

Elisha ndiye alikuwa nabii mpya. Aliamini Mungu. Mungu alimfanya nabii waajabu. Mungu alimpa nguvu na uwezo wake. Alikuwa na nguvu maradufu za Eliya. Alifanya miujiza mingi na hizo nguvu za Mungu. Alifundisha watu wengi juu ya Mungu na kuenenda kwa njia za Mungu.